**Shirika la CDC la Afrika Kuandaa Mkutano wa Uzinduzi wa Kila Mwaka kuhusu Afya ya Umma barani Afrika kuanzia tarehe 14 hadi 16 Desemba**

*Mkutano huu unaandaliwa wakati ambapo kuna haja kubwa ya kushughulikia masuala ya kutokuwa na usawa katika viwango vya afya na kuendeleza hatua zinazopigwa katika huduma za kushughulikia dharura, uthabiti wa mfumo wa afya na ubunifu wa kisayansi barani Afrika*

*Jisajili sasa katika www.cphia2021.com*

**ADDIS ABABA, Agosti 12 2021** - Vituo vya Udhibiti na Uzuiaji wa Magonjwa vya Afrika (Africa CDC) vimetangaza leo kuwa Mkutano wa Kwanza wa Kimataifa kuhusu Afya ya Umma (CPHIA), ambao uliahirishwa mapema mwaka huu kutokana na janga la COVID-19, sasa utafanyika kwa njia ya mtandao kuanzia tarehe 14 hadi 16 Desemba 2021. Mkutano huu unatoa jukwaa la kipekee kwa watafiti wa Kiafrika, viongozi na wadau kushiriki matokeo ya kisayansi na mitazamo kuhusu afya ya umma na kushirikiana katika masuala ya utafiti, ubunifu na afya ya umma barani.

Bado janga la COVID-19 ni tishio kubwa barani Afrika. Visa vya maambukizi vikiwa vimefikia watu milioni 7 na karibu watu 175,000 kupoteza maisha barani kote, tayari athari zake zimekuwa kubwa mno. Kuathiriwa kwa shughuli za kiuchumi na kijamii ambako kumesababishwa na janga la COVID-19 kumehatarisha hata zaidi maisha na mapato ya watu, hali ambayo huenda ikarudisha nyuma hatua za maendeleo ya miaka mingi zilizopigwa na binadamu.

“Bara la Afrika limeathiriwa sana na janga la COVID-19. Wakati huo huo, janga la COVID-19 limesababisha fursa ya kihistoria ya kubuni upya mazingira ya afya ya umma ambayo yanatimiza ruwaza ya kuhakikisha kuwa kila mtu anapata huduma za afya barani kote. Kwa pamoja, tunaweza kubuni mifumo ya afya na uwezo wa kutengeneza bidhaa za kukabiliana kwa ufanisi na hatari nyingi za kiafya,” alisema John Nkengasong, MSc, PhD, Mkurugenzi wa shirika la CDC barani Afrika . “Mkutano wa uzinduzi wa kila mwaka wa shirika la CDC la Afrika unatoa jukwaa ambalo linalenga kutumia maarifa, ujuzi na azma ya Waafrika ili kwa pamoja kutoa fursa ya kupatikana kwa mustakabali bora wa afya kwa kila mtu.”

Katika kipindi hicho cha siku tatu, hatua za kisayansi zilizopigwa zinazolenga usambazaji wa chanjo ya COVID-19, kuimarika kwa mifumo ya afya na mafunzo yaliyopatikana kutokana na kukabiliana na janga la COVID-19 zitaangaziwa kupitia mawasilisho ya mada kuu na ya jopo, vipindi vya wajumbe na kushirikisha watu wengine kwa lengo maalum la kukuza ujuzi kwa wataalamu chipukizi. Kamati ya Maandalizi inayojumuisha zaidi ya viongozi 15 wa afya kutoka bara lote la Afrika na ulimwenguni wanasaidia kubuni mwelekeo wa kimkakati wa mkutano huu.

Mwenyekiti Mwenza wa CPHIA na Naibu Chansela wa Chuo Kikuu cha Usawa wa Viwango vya Afya Duniani, Profesa Agnes Binagwaho, MD, M(Ped), PhD alisema kuwa: “Kwa kuleta pamoja baadhi ya viongozi wakuu katika sekta ya afya ya umma barani Afrika, mkutano huu utatoa

jukwaa la kukagua mafunzo yaliyopatikana kutokana na janga la COVID-19 na kubuni mifumo thabiti zaidi ya afya ambayo inaweza kukabiliana kwa ufanisi na majanga ya siku zijazo. Tunatarajia kuona viongozi chipukizi wa siku zijazo wakiwa kwenye mstari wa mbele katika kuboresha afya ya umma, elimu ya kisayansi na utafiti barani Afrika."

"Miezi 18 iliyopita imekuwa ya changamoto na maisha magumu – hasa kwa wanawake, wasichana na vikundi vingine vya watu waliotengwa – lakini ujumbe mmoja dhahiri umejitokeza: ili kujenga mustakabali bora na wenye usawa zaidi kwa Waafrika wote, tunahitaji uongozi wa Kiafrika na suluhu za Kiafrika," alisema Profesa Senait Fisseha, MD, JD Mwenyekiti Mwenza wa CPHIA na Mkurugenzi wa Mipango ya Kimataifa na Shirika la Susan Thompson Buffett. "Nimevutiwa sana na talanta na ujuzi mkubwa ambao tayari tunao kwenye bara letu, na kujivunia uongozi wa shirika la CDC la Afrika. Kupitia jukwaa hili la kipekee, tunaweza kupiga hatua ya kijasiri ili kuboresha huduma ya afya kwa watu wote."

Maelezo ya ziada kuhusu mkutano yatapatikana miezi ijayo. Washiriki wanakaribishwa kujisajili ili kuhudhuria mkutano katika www.cphia2021.com.

**Wasiliana na:**
Ouma Onyango
Global Health Strategies
oonyango@globalhealthstrategies.com

**Kuhusu Shirika la CDC la Afrika:**
Shirika la CDC la Afrika ni shirika maalum la kitaalamu la Muungano wa Afrika ambalo husaidia Nchi Wanachama katika juhudi za kuimarisha mifumo ya afya na kuboresha uchunguzi, ushughulikiaji wa dharura, uzuiaji na udhibiti wa magonjwa.Pata maelezo zaidi katika: http://www.AfricaCDC.org

**-- MWISHO--**